

WAKAAZI wa Shehia ya Kikadini Jambiani wameiomba Mamalaka ya kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kuanzisha ofisi japo ya mtu mmoja kama Sheha katika Shehia ili kuondoa tatizo la Rushwa vijijini

Wakitoa michango yao baada ya kupatiwa elimu juu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi katika skuli ya msingi Kikadini Wilaya ya Kusini Unguja.

Wakaazi hao wamesema iwapo ZAECA itahamia na kufanya makazi kama mjumbe wa Sheha wa Shehia mjini na vijijini itasaidia kwa wanyonge wasiomiliki simu kupata haki zao.

Afisa wa mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi zanzibar Safia Makame Ramadhan amesema tamaa na mmong'onyoko wa maadili ni miongoni mwa sababu za rushwa hivyo ameitaka jamii kukinai na wanachokipata.

Wakati huo huo afisa elimu wa zaeca **Saada Salum Issa** wakati akiwapatia elimu wakaazi wa shehia ya Jambiani Kibigija katika skuli ya maandalizi Sirajatil Munira amesema iwapo jamii na watumishi watakuwa wazalendo na kuumwa na rasilimali za nchi yao itasaidia kupungua kwa vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi zanzibar

Amesema kufanya udanganyifu na kupitia njia za mkato ni miongoni mwa njia za rushwa hivyo ameitaka jamii kuacha tabia hiyo ili kuwepo kwa maendeleo endelevu nchini.